

DAFTARI LA

MKUTANO

MKUU

MKUTANO
MKUU
UMEFIKA!

NI WAKATI WA KUIMARISHA USHUHUDA WAKO,
KUSONGA KARIBU NA YESU KRISTO NA KUPOKEA
UFUNUO BINAFSI.

"Mimi . . . nimesali kwamba mkutano huu utakuwa muda wa uhuishwaji wa kiroho kwa kila mmoja wenu. . . Na mkutano huu uwe muda wa amani na karamu ya kiroho kwenu. Na mtafute na kupokea ufunuo binafsi wakati wa vikao hivi."

Rais Russell M. Nelson¹

ULIZA,

“Ufunuo halisi kwa ajili ya maswali ya moyoni mwako utafanya mkutano huu kuwa wenye thawabu na usiosahaulika.”

Rais Russell M. Nelson²

NA KISHA SIKILIZA

Je, una maswali au mashaka katika akili yako sasa hivi? Labda una wasiwasi kuhusu kupata marafiki wazuri ambao watakuinua na kukutia moyo. Ungeweza kujiuliza jinsi ya kuboresha kujistahi kwako au kukumbuka utambulisho wako wa kiungu. Pengine unajaribu kuamua ni chuo kikuu gani utatuma maombi. Au yawezekana kuwa una wasiwasi wa kawaida tu kuhusu siku za usoni, kukiwa na vurugu na ghadhabu katika dunia.



UNAWAZA NINI AKILINI MWAKO?

Utapata mengi zaidi kutoka katika mkutano mkuu kama utayaweka maswali na wasiwasi wako akilini. Bwana atakusaidia kupata majibu unapofungua moyo wako na kuwasikiliza watumishi Wake.



Maswali:



Majibu:



"Mungu hakika ataheshimu maagano na ahadi Zake kwa kila mmoja wetu. Hatuhitaji kuwa na hofu kuhusu hilo. . . . Sisi tunafanya kadiri ya uwezo wetu lakini lazima tumwachie Yeye utawala juu ya baraka, zote za kimwili na za kiroho.

Mzee D. Todd Christofferson³

KUJIFUNZA KUPITIA DHAMIRA

Je, umepata dhamira zozote katika hotuba ulizosikia?
Kuna zozote ambazo ni muhimu kwako wewe sasa?

 Dhamira:

 Ina Maana Gani Kwangu Mimi:



SIO KATIKA MAANDISHI?

Hakuna aliyekuambia uandike mihtasari yako ya mkutano mkuu. Unaweza kuchora mihtasari kama mbadala, kama hiyo inakusaidia kuyakamata vyema mawazo yako. Fanya kile kinachofaa kwako!

HISIA ZANGU NA MISUKUMO





"Katika maneno hayo mawili—"Msikilize Yeye"—Mungu anatupatia mpangilio wa mafanikio, furaha na shangwe katika maisha haya. Inatubidi sisi *tusikilize* maneno ya Bwana, *kuyatii* hayo na *kufuata* kile Alichotuambia!"

Rais Russell M. Nelson⁴



HOTUBA PENDWA

Je, una hotuba unayoipenda uliyosikia katika mkutano huu mkuu? Fikiria kuandika jina la msemaji, na kile alichozungumza na kwa nini unaipenda sana.

MUDA WA KUTAFAKARI

Mara mkutano unapokuwa umekwisha, ni wakati wa kufanyia kazi mambo yale uliyoyasikia na kuhisi. Hapa kuna baadhi ya maswali ya kukuwezesha kuanza:

- Je, ni kitu gani kimoja ninachoweza kufokasi juu yake wakati ninaposonga mbele?
- Je, kuna kitu chochote katika maisha yangu ambacho ninahitaji kubadili?
- Ni kwa jinsi gani ninaweza kuimarisha ushuhuda wangu juu ya manabii walio hai?
- Ni kwa jinsi gani upendo wangu kwa Mwokozi unaweza kukua?
- Je, kuna vitu ninaweza kufanya ili kumsikiliza vyema Yeye katika maisha yangu ya kila siku?
- Maswali mengine uliyonayo:



“Ndiyo, tunapaswa kujifunza kutokana na yaliyopita na ndiyo, tunapaswa kujiandaa kwa ajili ya siku za baadaye. Lakini ni *sasa* tu tunaweza kufanya hivyo. *Sasa* ndiyo wakati tunapoweza kujifunza. *Sasa* ndiyo wakati tunapoweza kutubu. *Sasa* ndiyo wakati tunapoweza kuwabariki wengine.”

*Rais Russell M. Nelson*⁵

MIHTASARI

1. Russell M. Nelson, “Kuhubiri Injili ya Amani,” mkutano mkuu Apr. 2022 (*Liahona*, Mei 2022, 6–7).
2. Russell M. Nelson, “Ukweli Halisi, Mafundisho Halisi na Ufunuo Halisi,” mkutano mkuu wa Okt. 2021 (*Liahona*, Nov. 2021, 6).
3. D. Todd Christofferson, mkutano mkuu Apr. 2022 (*Liahona*, Mei 2022, 78).
4. Russell M. Nelson, “Msikilize Yeye,” mkutano mkuu Apr. 2020 (*Ensign* au *Liahona*, Mei 2020, 89).
5. Russell M. Nelson, “Sasa Ndiyo Wakati,” mkutano mkuu Apr. 2022 (*Liahona*, Mei 2022, 126).

© 2023 na Intellectual Reserve, Inc.
Haki zote zimehifadhiwa.

IDHINI YA KUCHAPISHA UPYA KIJITABU HIKI IMETOLEWA KWA MATUMIZI BINAFSI YASIMO YA KIBASHARA. HII INAJUMUISHA IDHINI KWA VIONGOZI WA KATA KUCHAPISHA IDADI NDOGO YA NAKALA KWA AJILI YA WALE WANAOWAHUDUMIA KATIKA NAFASI ZA MIITO YAO. VIJITABU SHARTI VICHAPISHWE KWA UKAMILIFU WAKE. HII HAJIJUMUISHI IDHINI YA KUJWEKA MTANDAONI, KUTUMIA TENA AU KUSAMBAZA NYENZO HIL MATUMIZI YOYOTE YA ZIADA YA NYENZO HII YANAHTAJI KUIDHINISHWA.

permissions.ChurchofJesusChrist.org

JE, UNAHITAJI NAKALA ZAIDI?

Pakua na uchapishe daftari hili kwenye
conference.ChurchofJesusChrist.org.

